



# jifunze kusoma

KILIMO BORA CHA MINAZI

KIONGOZI CHA MWALIMU

Kitabu cha Elimu ya Watu Wazima

# JIFUNZE KUSOMA

## Kilimo Bora cha Minazi

## Kitabu cha Pili

Kiongozi cha Mwalimu

**Wizara ya Elimu**

**1985**

**Haki ya kunakili ni ya Wizara ya Elimu, Tanzania 198**

Wafuatao walishiriki kuandika kitabu hiki:

| | | |
|---|---|---|
| Jumanne M. Mayoka | – | Wizara ya Elimu, Dar es Salaam |
| Mwamini K. Katundu | – | Wizara ya Elimu, Dar es Salaam |
| Mattayo Y.S. Machoya | – | Wizara ya Elimu, Dar es Salaam |
| Barnabas Kimenyi | – | Wizara ya Elimu, Kituo cha Kisomo cha Taifa Mwanza |
| Rukia Mohammed Issa | – | Idara ya Elimu ya Watu Wazima Zanzibar |
| Mbarouk Khamis Said | – | Ellimu, Pemba |
| Shabani J. Mlacha | – | Wizara ya Kilimo na Uendelezaji Mifugo, Ukulima wa Kisasa, Dar es Salaam |
| Omari M.I. Ngwawasya | – | Wizara ya Kilimo na Uendelezaji Mifugo, Ukulima wa Kisasa, Dar es Salaam |
| Simon M.A. Magaigwa | – | Wizara ya Kilimo na Uendelezaji Mifugo Mpango wa Taifa wa Uendelezaji Minaz Dar es Salaam |
| Mshana M. Mwikari | – | Wizara ya Kilimo na Uendelezaji Mifugo, Mpango wa Taifa wa Uendelezaji Minazi, Dar es Salaam |
| Yunus Rashid | – | Idara ya Elimu, Mafia |

**Kimepigwa Chapa Tanzania na Kiwanda cha Uchapaji cha Elimu ya Watu Wazima, Dar es Salaam.**

# UTANGULIZI

Kitabu hiki Kiongozi cha Mwalimu Kitabu cha Pili kimetungwa ili kumsaidia mwallimu kufundisha ipasavyo masomo yaliyomo katika kitabu cha Mwanakisomo Jifunze Kusoma Kilimo Bora cha Minazi, Kitabu cha Pili. Mambo ya msingi yanayohusu jinsi ya kuendesha majadiliano ya kila somo ambayo yanahitaji maelezo zaidi yametajwa, kinagaubaga.

Kwa hiyo ili kuweza kufundisha kikamilifu, Mwalimu anatakiwa kutimiza mambo haya:

1. Fundisha kwa kuzingatia yaliyomo katika Dibaji ya Kiongozi cha Mwalimu Jifunze Kusoma Kilimo Bora cha Minazi Kitabu cha Kwanza.

2. Umwone mwanakisomo kuwa ni mkulima anayejua kusoma, kuandika na hesabu kiasi na pia kwamba mkulima huyo anahitaji kutiwa hamasa ili awe na ari ya kupenda kujiendeleza zaidi katika fani ya Kilimo.

3. Katika Hatua ya kusoma, mwanakisomo apewe fursa ya kusoma mwenyewe pasipo msaada wako mwalimu. Iwapo atashindwa muombe mwanakisomo mwingine asome huku yule aliyeshindwa akisikiliza na kufuatisha kimya kimya maneno yanayosomwa.

4. Kuhusu masomo yanayoambatana na maonyesho kwa vitendo hakikisha kuwa zana na vifaa vyote vinavyohusika vimeandaliwa mapema na vipo katika hali nzuri. Maonyesho hayo yazingatie maadili yanayosisitizwa katika maonyesho kwa vitendo - Kiongozi cha Mwalimu Jifunze Kusoma Kilimo Bora cha Minazi Kitabu cha Kwanza.

5. Baada ya maonyesho kwa vitendo Mwalimu pamoja na Bwana Shamba watembelee wanakisomo mashambani ili kuhakikisha kuwa waliyojifunza wametekeleza ipasavyo.

6. Iwapo mwanakisomo atakosea, tumia lugha nzuri ambayo haitamkatisha tamaa na kumuudhi.

7. Mwanakisomo apewe mazoezi mengi ya kusoma na kuandika ili asirudie hali ya kutojua kusoma na kuandika. Imla na kujibu kwa kuandika maswali ya kila somo ni njia inayofaa kufanikisha mazoezi ya kuandika.

8. Mwalimu unapaswa kujiendeleza pia ili uweze kuwaendeleza wanakisomo unaowafundisha. Kwa hiyo jisomee vitabu mbalimbali vinavyohusu fani ya kilimo na pia shirikiana na Bwana Shamba ili akueleze jinsi ya kufanya baadhi ya mambo yanayokutatiza.

Kumbuka, kubuni njia nyingine muhimu anayopaswa kuwa nayo mwalimu. Kwa hiyo fikiri njia za kutatua matatizo ya kielimu pasipo kutegemea misaada kutoka mahali pengine.

# SOMO LA 1

**Kusudi la Somo:**

- Umuhimu wa Minazi
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi na hesabu

**Vielelezo na Vifaa:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za maneno - **Bwana, Bibi, Hawa, Wanaishi, Wanakijiji, Wameamua, Wameelewa, Pawa na Vinywaji**
- Kadi za silabi - **bwa na nywa.**

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Kuhusu umuhimu wa minazi. Mwalimu awaulize wanakisomo ni kwa nini wanalima minazi.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kuandika na ubao wa chaki, kadi za maneno, sentensi na silabi za somo.
- Kujenga maneno mapya kutokana na silabi walizojifunza.
- Kutunga sentensi kwa kutumia maneno waliyojifunza.
- Kusoma kitabuni:
- Katika hatua hii, mwalimu asome kwa sauti huku akitamka maneno kwa usahihi kufuata vituo na wanakisomo wakisikiliza na kufuatisha kimya kimya vitabuni mwao.
- Wanakisomo wasome kimya vitabuni mwao. Pita kuwasaidia wanakisomo wenye matatizo ya kusoma.
- Wanakisomo wasomeane wenyewe kwa wenyewe katika vikundi.
  Mwalimu azungukie kila kikundi kutoa msaada ikibidi.
- Wanakisomo wasome mmoja mmoja kwa sauti. Hakikisha kuwa wanatamka maneno kwa usahihi na kufuata vituo, akishindwa msaidie.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Mwalimu awaulize maswali yaliyomo katika kitabu cha mwanakisomo ili wayajibu kwa kusoma tu. Baadaye wajibu maswali hayo katika daftari zao.
- Mwalimu apite kusahihisha kazi zao.
- Mwalimu afanye masahihisho ya jumla ubaoni kwa kushirikiana na wanakisomo kisha wanakisomo wayanakili majibu sahihi katika daftari zao.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Kujumlisha na kutoa – mamia, makumi na mamoja
- Mwalimu awafundishe wanakisomo hesabu zinazohusu kutoa na kujumlisha mamia, makumi na mamoja (marudio ya kitabu cha kwanza).
- Mwalimu atoe mfano huu unaohusu kujumlisha:

$$\begin{array}{r} 163 \\ +216 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia:** Awaeleze kuwa tunajumlisha mamoja kwanza: 3 + 6 = 9
Halafu tunajumlisha makumi: 6 + 1 = 7
Mwisho tunajumlisha mamia: 1 + 2 = 3
Pia mwalimu atoe mfano huu unaohusu kutoa:

$$\begin{array}{r} 266 \\ -153 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia:** Awaeleze kuwa tunatoa mamoja kwanza: 6 − 3 = 3
Halafu tunatoa makumi: 6 − 5 = 1
Mwisho tunatoa mamia: 2 − 1 = 1

Toa mifano mingine ya namna hii mpaka wanakisomo wameelewa.
Angalia usitoe mifano inayohusu "Kukopa" k.m.

$$\begin{array}{r} 763 \\ -165 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

Pia epuka hesabu zinazohusu "Chukua" katika kujumlisha. k.m.

$$\begin{array}{r} 266 \\ +164 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

Hesabu zinazohusu "Kukopa" na "Chukua" ni mapema mno kwao.

**Maswali:**

1. Bwana na Bibi Mgeni walikwenda shambani kuvuna nazi. Siku ya kwanza walivuna nazi 165, siku ya pili nazi 134. Je, walivuna nazi ngapi kwa jumla?

2. Katika shamba la kijiji cha Upeo kuna minazi 856, minazi 146 imeshambuliwa na mdudu chonga. Je, minazi mizuri ni mingapi?

3. Bwana na bibi Mgeni waliuza nazi zao. Mwezi wa kwanza walipata shs.316. Mwezi wa pili walipata shs.433. Je, walipata shs. ngapi jumla?

4. Kijiji cha Upeo kilifyeka hekta 916. Hekta 604 zimelimwa. Je, hekta ngapi bado hazijalimwa?

## SOMO LA 2

**Kusudi la Somo:**

- Kwa nini minazi ni mali
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi na hesabu

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kuandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za maneno - **kadhalika, viwanda, vyao, nyumbani, hutegemea. vyombo,sabuni, mafuta, dawa na ghafi.**

- Kadi ya silabi – gha.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

: Kuhusu kwa nini minazi ni mali

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

Fuata njia ulizoonyeshwa katika somo la 1

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

Fuata njia ulizoonyeshwa katika somo la 1

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Mwalimu awafundishe wanakisomo hesabu zinazohusu kuzidisha na kugawa mamia, makumi na mamoja. (marudio ya kitabu cha kwanza).
  Atoe mfano huu.

$$\begin{array}{r} 123 \\ \times 3 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia:** Zidisha mamoja kwanza $3 \times 3 = 9$
Zidisha makumi $2 \times 3 = 6$

Zidisha mamia $1 \times 3 = 3$

- Toa mfano mwingine

$$\begin{array}{r} 124 \\ \times 2 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia:**
- Zidisha mamoja: $4 \times 2 = 8$
- Zidisha makumi: $2 \times 2 = 4$
- Zidisha mamia: $1 \times 2 = 2$

Hivyo: (i) $\begin{array}{r} 123 \\ \times 3 \\ \hline 269 \\ \hline \end{array}$ (ii) $\begin{array}{r} \text{Shs.}124 \\ \times 2 \\ \hline 248 \\ \hline \end{array}$

Atoe mfano unaohusu kugawa. Aeleze kuwa:
(a) Tunaanza kugawa mamia kwanza
(b) Halafu tunagawa makumi
(c) Mwisho tunagawa mamoja.

Mfano (i) $264 \div 2$

**Njia:** Mamia 2 gawa kwa 2 = 1
Makumi 6 gawa kwa 2 = 3
mamoja 4 gawa kwa 2 = 2

Mfano (ii) Shs.884 ÷ 4

**Njia:** Mamia 8 gawa kwa 4 = 2
Makumi 8 gawa kwa 4 = 2
mamoja 4 = 1

Hivyo (i) $264 \div 2 = 132$
(ii) Shs.884 ÷ 4 = 221

Mwalimu atoe mifano mingine inayohusu kuzidisha na kugawa. Angalia kuwa mifano hiyo inayohusu kuzidisha haihusu "chukua" au "peleka" k.m. 126 x 4 au katika kugawa inayohusu "baki"

k.m. $396 \div 2$

1. Kijiji cha Upeo kimepeleka mchango wa shs.642 kwenye ofisi ya Kata kwa ajili ya mafuta ya Mwenge.
Kama fedha hizi zimechangwa sawasawa na vitongoji viwili vya

kijiji kila kitongoji kimetoa kiasi gani?

2. Bibi Mgeni aliuza embe kwa siku 3 mfululizo. Kila siku aliuza embe 113. Je, aliuza embe ngapi jumla?

3. Kama alipata shs.636,Je kila siku alikuwa anapata shilingi ngapi?

## SOMO LA 3

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 1 na 2
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi, na hesabu.
- Kuandika na kutumia maneno mapya waliyojifunza katika somo la 1 na 2.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi.
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:** o – kuhusu marudio katika somo la 1 na somo la 2.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**
- fuata njia zilizoelezwa katika somo la 1.
- Mwalimu aandike sentensi katika somo la marudio toka sentensi ya kwanza hadi ya nne.

**Hatua ya Tatu:**

- Wanakisomo wafanye mazoezi ya maneno na silabi.

**Mazoezi:** Somo la 1
Silabi mpya zilizomo katika somo la 3.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**
- Hesabu za fedha: Kujumlisha, kutoa
- Mwalimu arudie hesabu za fedha zinazohusu kujumlisha na kutoa (marudio ya somo la 1 na 2).

**Mfano:** (i) Kujumlisha

| | shs. | Senti |
|---|---|---|
| | 21 | 50 |
| + | 47 | 35 |
| | 68 | 85 |

(ii) Kutoa

| | shs. | senti |
|---|---|---|
| | 47 | 50 |
| − | 21 | 35 |
| | 26 | 15 |

Toa mifano mingine ya namna hii.

2. Kijiji cha Upeo kinataka kujenga ofisi ya wazazi kwa njia ya kujitolea. Kitongoji kimoja kimefyatua matofali 1263. Kitongoji kingine kimefyatua matofali 4325. Je vitongoji vyote vimefyatua matofali mangapi?

3. Bwana na Bibi Mgeni wamenunua sare kwa ajili ya watoto wao 3. Bei ya kila sare ni shs.123.
Je Bwana na Bibi Mgeni watatoa shilingi ngapi?

4. Shule ya Msingi ya Upeo ina watoto 424. Kila mtoto anatakiwa kuchanga shs.2/= kwa ajili ya kununua mpira. Je, ni kiasi gani cha fedha kitakusanywa?

5. Idadi ya wakazi wa kijiji cha Upeo ni watu 1946. Kati yao 623 ni watoto. Je, watu wazima ni wangapi?

## SOMO LA 4

**Kusudi la Somo:**

- Mahitaji ya minazi
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi na maswali ya somo la nne.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi.
- Picha nambari 2.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu mahitaji ya minazi

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi, maneno na silabi za somo
- Fuata hatua za kusoma kama ilivyo katika somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali somo la nne katika kitabu cha mwanakisomo.
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Kujumlisha, kutoa na "kukopa" mamia, makumi na mamoja.
- Katika somo hili wanakisomo wafundishwe jinsi tunavyofanya hesabu za "kukopa" katika kutoa mamia, makumi na mamoja; na "kuchukua" katika hesabu za kujumlisha mamia, makumi na mamoja.

**Mfano:** (i) Kujumlisha

$$\begin{array}{r} 263 \\ +458 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

Hatua: Jumlisha mamoja 3 + 8 = 11 andika 1 chini ya 8, "chukua" kumi moja.

Jumlisha makumi 6 + 5 = 11, ongeza kumi 1 = 12 andika 2 chini ya 5 "chukua" mia 1.

Jumlisha mamia 2 + 4 = 6 ongeza mia moja = 7 andika 7 chini ya 4.

Hivyo:

$$\begin{array}{r} 263 \\ +458 \\ \hline 721 \end{array}$$

Toa mfano mwingine wa namna hii.

**Mfano:** (ii) Kutoa:

$$\begin{array}{r} 763 \\ -274 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

Toa mamoja 3 − 4 haiwezekani kwani 3 ni ndogo, chukua 1 katika 6 inakuwa 10 + 3 = 13. Hivyo 13 − 7 = 6

: Toa makumi 5 − 7 haiwezekani kwani 5 ni ndogo, chukua mia 1 katika mamia 7 inakuwa 10 + 5 = 15. Hivyo 15 ÷ 7 = 8. Andika 8 chini ya 7.

: Toa mamia 6 ÷ 2 = 4 Andika 4 chini ya 2.

- Eleza hatua hizi kwa utaratibu sana mpaka wameelewa. Toa mifano mingine ya kutosha kuhusu hesabu hizi.

**Maswali:**

1. Kwenye kitalu cha minazi kuna miche 863. Miche 274 imenunuliwa na wakulima. Je miche mingapi imebaki?

2. Katika kijiji chetu, tulinunua vifaranga. Mwezi wa kwanza tulinunua vifaranga 267 mwezi wa pili vifaranga 587. Je jumla kijiji kilinunua vifaranga vingapi?

3. Mhasibu wa kijiji chetu, aliuza bidhaa za duka la kijiji. Siku ya kwanza alipata shs.648; siku ya pili shs.262.
Je, Jumla alipata shilingi ngapi?

# SOMO LA 5

**Kusudi la Somo:**

- Aina za minazi
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi, hesabu na maswali ya somo la tano.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu aina za minazi.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi, maneno na silabi za somo la tano katika kitabu cha mwanakisomo.
- Fuata hatua za kusoma katika somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo la tano
- Fuata hatua za kujibu maswali kama ilivyoonyeshwa katika somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Kuzidisha na kugawa - hesabu zinazohusu "kuchukua" na "baki" katika kugawa.
  Mwalimu atoe mfano huu:–

(i) Kuzidisha:- 32
×6

---

Zidisha mamoja 2 × 6 = 12
Andika 2 chini ya 6; chukua kumi 1.
Zidisha makumi 3 × 6 = 18; ongeza na ile kumi uliyochukua 18 + 1 = 19.

(ii) 139
×8

---

: Zidisha mamoja 9 × 8 = 72; andika 2 chini ya 8, chukua kumi 7
: Zidisha makumi 3 × 8 = 24; ongeza ile kumi 7
= 24 + 7 = 31; andika 1 chini ya 3 chukua 3.
: Zidisha mia 1 × 8 = 8; ongeza 8 na 3 = 11

Hivyo (i) 32 ×6 = 192 (ii) 139 ×8 = 1112

Toa mifano mingine ya namna hii mpaka wanakisomo wame-elewa

(ii) **Kugawa:** 462 ÷ 3

Njia:– Mamia 4 gawa na 3 = 1 baki mia 1
: Chukua 1 ambayo ni vitu 10 ongeza na 6
: Gawa 16 – 3 = 5 baki; chukua 1 ambayo ni vitu 10, ongeza 2 = 12
: Gawa 12 ÷ 3 = 4.

Hivyo:– 3/462
154

Toa mifano mingine ya namna hii inayohusu kuzidisha na kutoa.

## SOMO LA 6

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 5
- Kufundisha kusoma na hesabu

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi,
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi za somo la marudio

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu somo la 4 na 5

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Fuata njia zilizoelezwa katika somo la 4.
- Mwalimu aandike sentensi kutoka katika somo la marudio toka sentensi:–
- Minazi ni ya aina mbili, minazi mirefu na minazi mifupi.
- Minazi mirefu huanza kuzaa baada ya miaka 7 hadi 10.
- Minazi mifupi huanza kuzaa baada ya miaka 3 hadi 4
- Minazi chotara ni mchanganyiko wa minazi mirefu na minazi mifupi.
- Aina zote za minazi zinafaa kama zinatunzwa vizuri.

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Wanakisomo wajadiliane katika vikundi kisha watoe taarifa zao za majadiliano. Baada ya hapo watoe taarifa zao za majadiliano. Baada ya hapo mwalimu aandike maelezo yaliyo sahihi kutokana na majadiliano ya vikundi na hatimaye wayaandike katika daftari zao.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Marudio ya somo la 4 na 5. Fanya mazoezi yanayohusu hesabu za kujumlisha, kutoa, kuzidisha, na kugawa kama ilivyoelezwa katika masomo yaliyopita, ukitunga mifano yako inayohusu:–

(i) Hesabu za kujumlisha mamia, makumi na mamoja zinazohusu "kuchukua"

k.m. 364
+478

(ii) Hesabu za kutoa zinazohusu "kukopa"

k.m. 473
−294

(iii) Hesabu za kuzidisha zihusuzo "kuchukua"

k.m. 212
×7

(iv) Hesabu za kugawa zinazohusu "Peleka"

k.m. 2/952

Mwalimu asome tarakimu zifuatazo halafu wanakisomo waandike katika madaftari yao.

1. Shs.456.65
2. Shs.506.95
3. 1263
−853
4. 617
+597
5. 99 × 3=
6. 963 ÷ 3=
7. 2562
−1257
8. Shs. 995.70
−750.60

9. 127 × 9 = 10. 396 − 9 =

Kisha watafute majawabu ya hesabu ya 3 − 10.

## SOMO LA 7

**Kusudi la Somo:**

- Hatari za moto
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi, hesabu na maswali

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo
- Picha nambari 3

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu hatari za moto

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi, maneno na silabi za somo la saba
- Fuata hatua za kujibu maswali ya somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Mwalimu awafundishe wanakisomo wazo la vipimo vya uzito (kilo), urefu (mita) na ujazo (lita). Aeleze.
  - (i) Vitu vina uzito. Tunajua uzito halisi wa kitu kwa kukipima katika mizani.
  - (ii) Uzito wa kitu huwa katika kilogram au kwa ufupi "kilo." Uzito mdogo sana ni gramu
  - (iii) Urefu wa kitu huwa katika **sentimita** na **mita**. Mita ni kipimo kirefu **zaidi** ya sentimita. Tunaweza kujua urefu halisi wa kitu kwa kutumia "mitatumbo"
  - (iv) Ujazo wa vitu kama vile mafuta, maziwa, maji, huwa katika **lita**.
- Mwalimu awaonyeshe wanakisomo mawe ya uzito wa kilo 1, 2, 5 n.k.

Achukue "mitatumbo" na awapime baadhi ya wanakis· mo kujua urefu wao.
Achukue chupa za ujazo mbali mbali za lita 1, nusu lita n.k.
Awaeleze wanakisomo kuwa debe moja la kawaida lina ujazo wa lita 20 na pipa kubwa ni lita 200

- Vipimo hivi vya uzito, urefu na ujazo ni muhimu sana kwa wanakisomo, hivyo tumia vitu halisi badala ya kuelezea tu.

**Eleza:**

(i) Uzito wa wastani wa mtu mzima ni kilo 50
(ii) Uzito wa wastani wa mtoto azaliwapo ni kilo 2.5
(iii) Urefu wa wastani wa minazi mirefu ni mita 15
(iv) Urefu wa wastani wa minazi mifupi ni mita 7 – 12

**Maswali:**

1. Uzito wa pamoja wa Bwana na Bibi Mgeni ni kilo 140. Kama Bibi Mgeni uzito wake ni kilo 80, Je Bwana Mgeni ana uzito gani?

2. Urefu wa kutoka shuleni hadi ofisi ya Chama ni mita 60, na kutoka ofisi ya Chama hadi ofisi ya Wazazi ni mita 85. Nini urefu toka shule hadi ofisi ya Wazazi.

3. Kijiji kiliuza maziwa kama ifuatavyo:–
Siku ya kwanza lita 25
Siku ya pili lita 27
Siku ya tatu lita 36
Je jumla lita ngapi ziliuzwa?

4. Bei ya lita moja ya maziwa ni shs.9.
Kijiji kiliuza lita 72. Je Kijiji kilipata fedha kiasi gani?

5. Bei ya kilo moja ya nyama ni Shs.50/= Bibi Mgeni alinunua kilo 3 alilipa kiasi gani?

## SOMO LA 8

**Kusudi la Somo:**

- Kupalilia
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi, hesabu na maswali

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo
- Picha nambari 4.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu athari za magugu na jinsi ya kupalilia.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi, maneno na silabi za somo la nane
- Fuata hatua za kusoma, somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Hatua za kujibu maswali, somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Vipimo vya uzito, urefu na ujazo limeendelea. Somo hili liwe la vitendo ili kutilia mkazo wazo la urefu.

  (i) Wapime na kujua urefu na upana wa majengo yaliyopo k.m. Majengo ya shule, nyumba zilizo jirani n.k.

  (ii) Urefu wa kutoka sehemu moja hadi nyingine.
  (iii) Jadiliana na wanakisomo kuhusu uzito wa vitu mbali

mbali.

k.m. (a) Je uzito wa debe moja la mpunga au mahindi lililojaa ni kilo ngapı? Kama wanakisomo wakisema kilo 200 au 90 jadiliana kuwa kwa nini siyo sahihi

(b) Je uzito wa gunia moja la unga wa mahındi ni kilo ngapi?

Mwalimu anapaswa kuwa na majibu sahihi kwa maswali ya uzito wa debe lililojaa unga au nıpunga;
Uzito sahihi wa gunia la unga lililojaa. Fanya utafiti kabla hujaanza kufundisha sehemu hii.

Wanakisomo washike vitu mbali mbali na kukadiria uzito wake.

**Maswali:**

1. Gunia la sukari lina uzito wa kilo 50 Je magunia 3 yatakuwa na uzito gani?

2. Gunia kubwa la unga lina uzito wa kilo 100 je magunia 4 yana uzito gani?

3. Mgeni alitengeneza mafuta ya nazi lita 20. Akauza lita 11. Je zilibaki lita ngapi?

4. Urefu wa kamba ni mita 24. Kama bei ya mita 1 ni Shs.3 Je bei ya yote ni nini.

## SOMO LA 9

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 7 na 8
- Kufundisha kusoma sentensi na hesabu za somo la marudio.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi za somo
- Picha nambari 3 na 4.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu marudio ya somo la 7 na 8

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi za somo la marudio 7 na 8
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la marudio katika kitabu cha mwanakisomo.
- Fuata hatua za majadiliano za somo la sita.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Marudio ya somo la 7 na 8
- Rudio vipimo vya uzito - kilo
- Rudia vipimo vya urefu - mita
- Rudia vipimo vya ujazo - lita.

Mwalimu asome kwa sauti ya kusikika yafuatayo halafu wanakisomo wanakili katika madaftari yao.

1. Kilo 124
2. Lita 1256
3. Mita 2864
4. Miche 3956
5. Minazi 703.

**Maswali:**

1. Katika Kijiji cha Upeo kuna vitalu 2 vya aina ya minazi mirefu, miche 1364, minazi mifupi 2556. Je vitalu vyote vina miche mingapi?
2. Bwana na Bibi Mgeni wamefuga kuku wa mayai 456 kila kuku anataga yai 1 kila siku je kwa siku 2 Bibi Mgeni atakusanya mayai mangapi?
3. Shule ya Msingi ya Upeo imefuga ng'ombe 2 wa maziwa. Kila ng'ombe hutoa lita 12 kwa siku. Je ng'ombe hao 2 wanatoa lita ngapi kwa siku?
4. Urefu wa choo unatakiwa uwe mita 6. Mgeni amechimba urefu wa mita 4. Je bado kuchimba mita ngapi?
5. Mtoto mmoja wa shule hukaa umbali wa mita 1,000 toka shule. Je kwenda na kurudi anasafiri mita ngapi?

## SOMO LA 10

**Kusudi la Somo:**

- Faida ya kuchanganya mazao.
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi, hesabu na Maswali

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo
: Picha nambari 5.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu - faida za kuchanganya mazao

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi, maneno na silabi za somo
- Fuata hatua za kusoma, somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali, somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- mwalimu awafundishe wanakisomo wazo la "tani" kilomita na hekta.

**Aeleze:** (i) Kipimo kilicho kizito zaidi ya kilo ni **tani.**
Kilo 1,000 ni sawa na tani 1.
**Hivyo:** Kilo 2,000 ni sawa na tani 2
Kilo 3,000 ni sawa na tani 3

(ii) Kipimo kilicho kirefu zaidi ya mita ni **Kilomita** (km)
Mita 1,000 ni sawa na kilomita 1
Mita 2,000 ni sawa na kilomita 2
Mita 3,000 ni sawa na kilomita 3

(iii) Kipimo cha eneo huitwa hekta. Hekta moja ni mita 100 x 100 yaani mita za eneo 10,000.

Katika hekta moja unaweza kupanda miche 154 kwa hatua ya m.9 kwa m.9.
Unapofundisha "Hekta" fanya kwa vitendo ili wanakisomo wawe na wazo la hekta kuona ni eneo la kiasi gani.

**Maswali:**

1. Kijiji cha Upeo kimenunua lori lenye uzito wa tani 9. Je uzito wa lori hilo ni sawa na kilo ngapi?

2. Katika kijiji cha Upeo hadi Kijiji cha jirani ni kilomita 6. Je ni sawa na mita ngapi?

3. Shule ya Msingi ya Upeo wana hekta 1 ya minazi. Wamepanda minazi 154 katika hekta hiyo. Kama kila mche wa mnazi ni Sh.10. Je shule hiyo ililipa kiasi gani?

4. Kijiji cha Upeo kimefyatua matofali 2862 siku ya kwanza, na matofali 4,892 siku ya pili. Je jumla ni matofali mangapi?

5. Bwana na Bibi Mgeni walikusanya nazi 3647 katika mwaka wa kwanza, na nazi 2564 mwaka wa pili. Jumla walikusanya nazi ngapi?

6. Lori la Kijiji cha Upeo lilikwenda kusomba matofali ya Kijiji. Jumla ya matofali ni 22384. Lilikwenda mara mbili na kila safari lilichukua idadi ile ile. Je kila safari lilichukua matofali mangapi?

7. Tani moja ya muhogo mbichi hutoa wastani wa kilo 300. Kijiji cha Upeo kina tani 9 za muhogo mbichi. Je tani hizo zitatoa kilo ngapi?

## SOMO LA 11

**Kusudi la Somo:**

- Faida na matumizi ya mbolea
- Kufundisha kusoma, sentensi, maneno, silabi, hesabu na maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo
- Picha nambari 6.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**
- Majadiliano kuhusu faida na matumizi ya mbolea.

**Hatua ya Pili:**
**Kusoma:**
- Kusoma sentensi, maneno na silabi za somo.
- fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali, somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Marudio ya somo la 11

- Marudio ya somo la 10: Uzito kg na Tani
  kg. 1,000 = Tani 1
  Urefu mita wa kilomita
  m.1,000 = km.1

Eleza: Kilo 1,000 = Tani
: Kilo 1,250 = Tani 1¼ (Tani moja na robo)
: 1,500 = Tani 1½ (Tani moja na nusu)
: Kilo 1,750 = Tani 1¾ (Tani moja na robo tatu)

: Meta 1,000 = Kilomita 1
: Meta 1,250 = Kilomita 1½
: Meta 1,750 = Kilomita 1¾

Eleza: Kilo 250 = ni sawa na robo tani
: Kilo 500 = ni sawa na nusu tani
: Kilo 750 = ni sawa na robo tatu tani

Eleza: Meta 250 = robo kilometa
: Meta 500 = nusu kilometa
: Meta 750 = robo tatu kilometa

Mwalimu awaeleweshe wanakisomo yafuatayo halafu waandike katika madaftari yao.

## SOMO LA 12

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 10 na 11
- Kufundisha kusoma na sentensi na hesabu za somo.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi za somo la 12
- Picha nambarı 5 na 6

**Jinsi ya Kufundisha Somo**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu somo la 10 na 11

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi za somo la marudio
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 12

- Fuata hatua za majadiliano za somo la 6

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

- Marudio ya somo la 10 na 11
- Wakumbushwe wanakishomo kuhusu vipimo vya
  - (i) Uzito - kilo (kg) na tani (Ta).
  - (ii) Urefu - mita na kilomita (km)
  - (iii) Hekta
  - (iv) lita.

**Eleza:** (i) Tukitaka kujua uzito wa kitu tunakipima kwa kutumia **mizani**
- Tukisha kipima uzito wake kuwa kilogram (kilo)

- Kilo 1,000 ni sawa na Tani 1

(ii) Tukitaka kujua urefu wa kitu tunakipima kwa kutumia **"mita-tumbo"**
- Tukisha kipima urefu wake huwa katika mita.
- Mita 1,000 sawa na kilomita 1.

(iii) Maeneo ya mashamba huwa katika vipimo vya hekta.
- Katika hekta moja unaweza kupanda minazi 143 kwa vipimo vya mita 9 kwa mita 9.

(iv) Tukitaka kujua ujazo wa vitu kama vile maji, mafuta, asali, maziwa tunatumia vipimo vya **lita**.
- Chupa ya bia ni **nusu lita**
- Ng'ombe wa kisasa wa maziwa akitunzwa vizuri anaweza kutoa lita 10 - 15 kwa siku.
- Ng'ombe wetu wa kienyeji hutoa lita 1au 2 kwa siku.

**Maswali:**

1. Kijiji cha Upeo kilipeleka bidhaa zifuatazo ili zikauzwe:
   Mbata tani 1263
   Mhogo tani 4564
   Je jumla walipeleka tani ngapi?

2. Lori la Kijiji husafiri kilomita 150 kila siku.
   Je kwa siku 9 litakuwa limesafiri kilomita ngapi?

3. Kuna watoto 45 katika darasa. Kama kila mtoto atapewa kamba yenye urefu wa mita 2. Jumla watakuwa na kamba ya urefu gani?

4. Ng'ombe wa kisasa hutoa lita 15 kwa siku. Je kwa siku 12 atatoa lita ngapi?

## SOMO LA 13

**Kusudi la Somo**

- Kutandaza nyasi/majani makavu
- Kufundisha kusoma na sentensi, maneno, silabi, hesabu na maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo.
- Picha nambari 7.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu kutandaza nyasi/majani makavu shambani

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi maneno na silabi za somo.
- Fuata hatua za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Mwalimu awafundishe wanakisomo vipimo vidogo vya **uzito** na **urefu** ambavyo ni:–

(i) Uzito - gramu
(ii) Urefu - sentimita

**Aeleze:** (i) Kuna kipimo kidogo cha uzito huitwa gramu
– gramu 1,000 ni sawa na kilo 1

(ii) Kipimo kidogo cha urefu huitwa sentimita
– sentimita 1,000 ni sawa na mita 1.

**Hivyo:** Gramu 1000 ni sawa na kilogramu 1
Gramu 1250 ni sawa na kilogramu 1¼
Gramu 1500 ni sawa na kilogramu 1½
Gramu 1750 ni sawa na kilogramu 1¾

Endelea hivi hivi kuonyesha kuwa:

Sentimita 1,000 ni sawa na mita 1
Sentimita 1,250 ni sawa na mita 1¼
Sentimita 1,500 ni sawa na mita 1½
Sentimita 1,750 ni sawa na mita 1¾

## SOMO LA 14

**Kusudi la Somo:**

- Kuzuia chonga
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi. hesabu na kujibu maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo
- Picha nambari 8.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu jinsi ya kuzuia Chonga.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi maneno na silabi za somo.
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo lakwanza.

Kuzidisha na kugawa kwa 10, 100 na 1,000

Mfano: (i) Kuzidisha 2 x 10 = 20 au 10 + 10
2 x 100 = 200 au 100 + 100
2 x 1000 = 2000 au 1000 + 1000

Waonyeshe wanakisomo kuwa tunapo zidisha kwa 10, tunaweka

sifuri nyuma ya tarakimu.

100, tunaweka sifuri nyuma ya tarakimu
1000 tunaweka sifuri tatu nyuma ya tarakimu

Mfano: (ii) Kugawanya:

20 ÷ 10 = 2 eleza kuwa sifuri nyuma ya 2 inaachwa
200 ÷ 100 = 2 sifuri mbili nyuma ya 2 zinaachwa
2000 ÷ 1000 = 2 sifuri tatu nyuma ya 2 zinaachwa.

**Toa mifano mingine:**

13 x 10 = 130
13 x 100 = 1300
13 x 1000 = 13000

Mwalimu asome mafumbo yafuatayo halafu wanakisomo wandike majawabu.

1. 14 x 10 = 2. 17 x 10 = 3. 15 x 100 = 4. 12 x 10 =

5. 7 x 10 = 6. 8 x 100 = 7. 13 x 1000 =

# SOMO LA 15

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 13 na 14
- Kufundisha kusoma sentensi na hesabu

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi ya sentensi za somo la 15
- Picha nambari 7 na 8

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu somo la 13 na 14.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi za somo la 15.
- Fuata hatua za kusoma somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 15
- Fuata hatua za majadiliano za somo la 6.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

**Marudio:**

- Rudia somo la 13 na 14. Mkazo uwe juu ya vipimo ambavyo hutumika sana, gramu sentimita.
  Onyesha njia ya kuzidisha kwa 10, 100, 1000 kama ilivyoelezwa katika masomo hayo.

## SOMO LA 16

**Kusudi la Somo:**

- Kupandikiza minazi katika shamba la zamani
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, hesabu na kujibu maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- kadi za sentensi, maneno hesabu na kujibu maswali.

**Jinsi ya kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu kupandikiza miche ya minazi katika shamba la zamani.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi na maneno ya somo.
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza.

**Hesabu:**

Kuzidisha kwa njia ndefu.
Toa mfano huu 13 x 25

$$\begin{array}{r} 13 \\ \times 25 \\ \hline \end{array}$$

**Njia:** Zidisha mamoja 5 x 3 = 15
Andika 5 chini ya 5 chukua 1

Zidisha makumi 1 x 5 = 5, ongeza na ile 1 = 6, Andika chini ya 2
Zidisha 2 x mamoja 3 = 6, Andika 6 chini ya 2
Zidisha maalum 1 x 2 = 2, andika chini ya alama x.

**Hivyo:**

```
   13
  ×25
 ----
   65
  260
 ----
  325
 ----
```

Jumlisha:

```
   65
 +260
 ----
  325
 ----
```

Toa mfano mwingine:

```
   78
  ×26
 ----
```

**Njia:** Zidisha mamoja 8 x 6 = 48

Andika 8 chini ya 6, chukua 4
Zidisha makumi 7 x 6 = 42 jumlisha na ile 4 = 46.
Andika 2 mara mamoja 8 = 16, Andika 6 chini ya 6 chukua 1.
Zidisha makumi 7 x 2 ongeza na ile 1 = 15
Andika 15 chini ya 4 weka 0 chini ya 8, halafu jumlisha.

Hivyo:

```
   78
  x26
 ----
  468
 1560
 ----
 2028
 ----
```

**Eleza kwa uangalifu sana jinsi tunavyopanga tarakimu hizi. Toa mifano mingine na fanya mifano hiyo na wanakisomo.**

## SOMO LA 17

**Kusudi la Somo**

- Kutayarisha shamba jipya la minazi.
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi, hesabu na kuji maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo
- Picha nambari 10

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu kutayarisha shamba jipya la minazi.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sent maneno na silabi za somo.
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Kuzidisha kwa njia ndefu inaendelea.

Mfano: $\begin{array}{r} 216 \\ \times\ 13 \\ \hline \end{array}$

Njia: Zidisha 6 x 3 = 18 Andika 8 chini ya 3 chukua 1.
: Zidisha 1 x 3 = 3 jumlisha na 1 = 4 Andika 4 chini ya 1.
: Zidisha 2 x 3 = 6 Andika chini ya alama x.
: Zidisha 6 x 1 = 6
: Zidisha 1 x 1 = 1
: Zidisha 2 x 2 = 2

**Hivyo:**

```
  216
 ×13
-----
  648
 2160
-----
 2708
-----
```

Toa mfano mwingine. Eleza jinsi tunavyopanga tarakimu hizi tunazo-zidisha. Fundisha jinsi ya kuzidisha makumi na mamoja kwa 20, 30, 40, 50, n.k.

**Mfano:** 24 x 20 =

```
  24
 x20
-----
```

Teremsha "0" halafu zidisha 4 x 2 = 8
2 x 2 = 4

Hivyo: jawabu ni 480

**Waeleze** pia 24 x 20 : zidisha 24 x 2, halafu weka sifuri nyuma ya **jawabu.**

Mfano: 133 x 30 =
133 x 3 = 399
Weka "0" nyuma ya 399 unapata 3990

Toa mifano mingine ya kuzidisha kwa 40, 50, n.k.

jawabu.

## SOMO LA 18

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 16 na 17
- Kufundisha kusoma sentensi na hesabu za somo la 188

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi za somo
- Picha nambari 9 na 10

**Jinsi ya Kufundisha:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu somo la 16 na 17

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki

Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 18
- Fuata hatua za majadiliano za somo la 6

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

**Marudio:**

- Kuzidisha kwa njia ndefu
  - (i) Makumi na mamoja. Kuzidisha na namba yenye tarakimu mbili k.m. 75 x 17
  - (ii) Mamia, makumi na mamoja. Kuzidisha na namba yenye

tarakimu mbili.
k.m. 236 x 27

Fanya na wanakisomo hesabu hizi:

| | | |
|---|---|---|
| 34 | 56 | 259 |
| × 24 | × 65 | × 43 |
| _____ | _____ | _____ |
| _____ | _____ | _____ |

(iii) Kuzidisha namba ambazo kizidishe kina sifuri
k.m. 17 x 30: waonyeshe jinsi ya kupanga:

17
x 30
_____

Fanya hesabu hizi:

63 X 40 = 39 X 50 = 26 X 80 =

## SOMO LA 19

**Kusudi la Somo:**

- Upimaji wa mashimo
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, hesabu na maswali

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi na maneno ya somo.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu upimaji wa mashimo

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi na maneno ya somo.
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

**Kalenda:** siku, wiki, mwezi na mwaka.
**Eleza:** Mwaka mmoja umegawanyika katika siku, wiki, na miezi

Siku **saba** hufanya wiki 1
Wiki nne hufanya mwezi 1
Miezi kumi na mbili hufanya mwaka 1.
Mwaka mmoja una wiki 52

Mwaka mmoja una siku 365 au 366

Fundisha: Siku: Jumatatu
Jumanne
Jumatano
Alhamisi
Ijumaa
Jumamosi
Jumapili

**Maswali:**

1. Bwana na Bibi Mgeni wamelima shamba lao kwa muda wa siku 35. Je ni wiki ngapi hizo?

2. Kijiji cha Upeo kimeamua kumaliza shamba lao la kijiji kwa muda wa wiki 6. Je ni siku ngapi hizo?
(6 × 7 = 42£.

3. Shule ya Msingi ya Upeo ina mihula mitatu.
Mihula yote ni wiki 36. Je ni siku ngapi hizo? (36 × 7 = 252). ).

## SOMO LA 20

**Kusudi la Somo:**

- Kuchimba mashimo
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, hesabu na kujibu maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi na maneno ya somo

: Picha nambari 11.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu namna ya kuchimba mashimo.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi, ubao wa chaki, sentensi na maneno ya somo.
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Kalenda miezi, mwaka

**Eleza:** Miezi na siku za kila mwezi.

**Miezi:** Januari siku 31

Februari siku 28
Machi siku 31
April siku 30
Mei siku 31
Juni siku 30
Julai siku 30
Agosti siku 31
Septemba siku 30
Oktoba siku 31
Novemba siku 30
Desemba siku 31

Fundisha kuwa mwezi Februari huwa na siku 28 au 29.
Eleza miaka ambayo mwezi Februari huwa na siku 29.
Katika mwaka mrefu mwezi Februari huwa na siku 29.

**Maswali:**

1. Umri wa mnazi mrefu ni miaka 90. Je ni karibu siku ngapi? (365 × 90 au 366 × 90)

2. Miezi yenye siku 30 iko 4. Je miezi hiyo ina siku ngapi? (30 × 4)

3. Miezi yenye siku 31 iko 7. Je miezi hiyo yote ina siku ngapi? (31 × 7)

4. Azimio la Arusha lilitangazwa mwaka 1967.
   Mpaka mwaka 1996 itakuwa ni miaka mingapi ( 1997 )
   ( 1967 )

5. Tanzania ilipata uhuru mwaka 1961. Je mpaka mwaka 1997 itakuwa miaka mingapi? ( 1997 )
   ( 1961 )

# SOMO LA 21

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya Somo la 19 na 20
- kufundisha kusoma sentensi na hesabu

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi za somo
- Picha nambari 11

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano somo la 19 na 20

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi za somo la 21
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la marudio la 21.
- Fuata hatua za majadiliano za somo la 6.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

**Marudio:**

Siku miezi mwaka.

Siku 7 ni sawa na wiki 1
Wiki 4 ni sawa na mwezi 1

Miezi 12 ni sawa na mwaka 1
Wiki 52 ni sawa na mwaka 1
Siku 365 au 366 ni sawa na mwaka 1

**Miezi ifuatayo ina siku 30**

Aprili
Juni
Septemba
Novemba

**Miezi ifuatayo ina siku 31**

Januari
Machi
Mei
Julai
Agosti
Oktoba
Desemba

Mwezi Februari huwa na siku 28 katika mwaka mfupi na siku, 29 katika mwaka mrefu.

Katika miaka ifuatayo mwezi Februari una siku 29, 1984, 1988 1992, 1996

**Maswali:**

1. Bibi Mgeni huuza maziwa lita 5 kila siku. Je katika mwaka 1984 aliuza lita ngapi katika mwezi Januari na Februari?

Idadi ya siku ni 31 + 29 = 60

Hivyo aliuza lita 60 X 5 = 300.

2. Kama kila lita ni shs. 10. Je alipata fedha kiasi gani katika miezi hiyo ya Januari na Februari mwaka huo wa 1984?

   Jumla ya lita ni 300
   Bei ya lita 1 ni shs.10/=

   Hivyo alipata shs.300 X 10 = 3,000/=

3. Bwana na Bibi Mgeni wanahudhuria masomo ya Elimu ya Watu Wazima toka Jumatatu hadi Ijumaa. Je ni siku ngapi hizo?

# SOMO LA 22

**Kusudi la Somo:**

— Kuweka mbolea
— Kufundisha kusoma sentensi, maneno- SAFI, ILIYONYOOKA hesabu na maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

— Ubao wa kubandika kadi
— Ubao wa chaki
— kadi za sentensi na maneno ya somo.

**Jinsi ya Kufundisha:**
**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

— Majadiliano kuhusu uwekaji mbolea

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

— Kama somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

— Kama somo la kwanza

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Kujumlisha, kutoa, kuzidisha na kugawa maelfu, mamia, makumi na mamoja.
Mwalimu awafundishe wanakisomo hesabu zihusuzo kujumlisha kutoa, kuzidisha na kugawa tarakimu zikiwa katika maelfu, mamia, makumi na mamoja.

Mfano (i) Kujumlisha

$$\begin{array}{r} 1343 \\ +4967 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Njia:** Fundisha kuwa tunaanza kujumlisha mamoja, halafu makumi, halafu mamia na mwisho maelfu.

**HIVI:** 3 + 7 = 10 Andika 0 chukua 1.
4 + 6 = 10 onyesha na 1 = 11 andika 1 chukua 1
3 + 9 = 12 ongeza 1 = 13 andika 3 chukua 1
1 + 4 = 5 ongeza 1 = 6.

Mfano (ii) Kutoa:

$$\begin{array}{r} 4967 \\ -1343 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

Njia: Toa mamoja kwanza, halafu toa makumi, kisha mamia na mwisho maelfu.

**HIVI:** 7 − 3 = 4
6 − 4 = 2
9 − 3 = 6
4 − 1 = 3

Jawabu ni 3624

(iii) **Kuzidisha:**

$$\begin{array}{r} 2344 \\ \text{x} \quad 2 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

Njia: Zidisha kwanza mamoja: 4 x 2 = 8 kish
Zidisha makumi : 4 x 2 = 8 kisha
Zidisha mamia : 3 x 2 = 6 kisha
zidisha maelfu : 2 x 2 = 4

**Jawabu ni 4688**

Kama kuna kuchukua, tumia njia ile ile uliyotumia nyuma.

(iv) Kugawa: 2 /2344

**Njia:** Gawa kwanza maelfu : 2 ÷ 1 halafu
Gawa mamia : 3 ÷ 2 = 1 baki 1 peleka 1 katika upande wa kulia inakuwa 14. 14 ÷ 2 = 7 mwisho.

## SOMO LA 23

**Kusudi la Somo:**

- Kupandikiza miche.
- kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi, hesabu na maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo.
- Picha nambari 12.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

. Majadiliano kuhusu upandikizaji wa miche.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kama somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kama somo la kwanza

**Hatua ya nne:**

**Hesabu:**

**Wakati:** Saa na dakika

Wanakisomo waweze kuelewa idadi ya masaa katika siku moja, na idadi ya dakika katika saa moja

Dakika 60 ni sawa na saa 1
Saa 24 ni sawa na siku 1.
Wafundishe wanakisomo juu ya:

(i) Nusu saa yaani dakika 30
(ii) Robo saa yaani dakika 15
(iii) Saa moja kasorobo au dakika 45

**Asubuhi:** Toka saa 1 - 6 masaa 6
**Adhuhuri:** Toka saa 7 - 9 masaa 3
**Jioni:** Toka saa 10 - 12 masaa 3

Hivyo mchana una saa 12 na usiku saa 12. Usiku na mchana hufanya siku moja au **saa 24.**

Dakika 60 = saa 1
Dakika 65 = saa 1 na dakika 5
Dakika 70 = saa 1 na dakika 10
Dakika 90 = saa 1 na dakika 30 au saa moja na nusu.
Dakika 120 = saa 2

**Maswali:**

1. Halmashauri ya Tawi la kijiji cha Upeo ilikaa kwa muda wa saa 1 na dakika 20.
   Je hizo ni dakika ngapi?
2. Mtoto mdogo wa Bwana na Bibi Mgeni hulala kwa saa 8 kila siku.
   Je hizo ni dakika ngapi?
3. Wanakijiji cha Upeo hulima katika shamba la ushirika kwa muda wa saa 7. Je hizo ni dakika ngapi?
4. Dereva wa kijiji hufanya kazi saa 8 kila siku. Kama kijiji kinalipa shs.3/= kila saa, Je hupata shs. ngapi kwa saa hizo 8?

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 22 na 23
- Kufundisha kusoma sentensi na hesabu

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi za somo
- Picha nambari 12

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 22 na 23

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kama somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 24
- Fuata hatua za majadiliano za somo la 6

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**
**Marudio**

- Wakati - dakika na saa, siku, wiki, miezi, mwaka.
- Uzito: gram, kilo, tani.
- Urefu: sentimita, mita, kilomita.
- Ujazo: lita
- Eneo: hekta.

**Wakati** - dakika 60 = saa 1

saa 24 = Siku 1
Siku 7 = wiki 1
Wiki 4 = mwezi 1
Miezi 12 = mwaka 1
Siku 365 au 366 = mwaka 1

**Majina ya miezi:**

Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba, Desemba.

Rudia miezi yenye siku 30 na 31. Rudia miaka ambayo Februari unakuwa na siku 29.

**Jadili:** Miezi ambayo Kijiji kinatayarisha mashamba.

**Urefu:** Sentimita, mita, kilomita
sentimita 1,000 = mita 1
Mita 1,000 = kilomita

**Jadili:** Urefu wa vitu mbali mbali ambavyo urefu wake unaweza kuwa katika sentimita na mita.
Urefu wa kutoka Kijiji cha Upeo hadi Kijiji au Vijiji vya jirani

**Uzito:** Gram na Kilogram - Tani
Gram 1,000 = kilogram 1
Kilogram 1,000 = Tani 1.

**Jadili:** Uzito wa vitu mbalimbali katika gram na kilogram. Kama kuna mizani kijijini wanakisomo wajipime ili kila mwanakisomo ajue uzito wake.

**Eleza:** Uzito wa magari ni katika kilo au Tani. Gari la tani 1 ni sawa na kilo 1,000, gari la tani 7 ni sawa na kilo 7,000.

**Ujazo:** Kipimo cha vitu vinavyotiririka k.m. maji, maziwa, mafuta, tunatumia lita.

**Eneo:** Tunatumia hekta au eka. Katika hekta 1 tunaweza kupanda minazi 154 kwa kutumia mita 9 kwa mita 9 kati ya mche na mche.

**Maswali:**

1. **Gari la Kijiji cha Upeo lina uzito wa tani 9. Je hizo ni sawa na kilo ngapi?**

2. Kijiji cha jirani kimelima hekta 10 na kupanda minazi. Kama hekta 1 ni minazi 154, Je hekta 10 kuna minazi mingapi?

3. Bei ya lita 1 ya asali ni shs.25, Je nini bei ya lita 15?

## SOMO LA 25

**Kusudi la Somo:**

- Wadudu washambuliao minazi
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, hesabu na kujibu maswali

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi na maneno ya somo

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu wadudu washambuliao minazi

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi na maneno ya somo la 25 kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki.

- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali ya somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

**Marudio:**

- Kujumlisha, kutoa, kuzidisha, na kugawa maelfu, mamia, makumi na mamoja.
- Wakati - Saa na dakika.

(i) Rudia hesabu za kujumlisha na kutoa:

(a) **Kujumlisha**

```
  9163
+ 2967
------
------
```

Jumlisha Mamoja
Jumlisha: Makumi
Jumlisha: Mamia
Jumlisha: Maelfu

(b) **Kutoa**

```
  9163
- 2967
------
------
```

Toa: Mamoja
Toa: Makumi
Toa: Mamia
Toa: Maelfu

Hakikisha kuwa wanaelewa sehemu za "Kuchukua" na "Kukopa"

(c) Kuzidisha

```
3633
x  3
----
----
```

Zidisha: Kwanza mamoja
Zidisha: Makumi
Zidisha Mamia
Zidisha: Maelfu

(d) Kugawa

```
3/3633
------
```

**Gawa:**
Maelfu
Mamia
Makumi
Mamoja

(ii) Rudia wakati na kalenda.
Mwaka - miezi - Juma - Siku - Saa - Dakika

Dakika 60 = Saa 1
Saa 24 = Siku 1
Siku 7 = Wiki 1
Wiki 4 = Mwezi 1
Miezi 12 = Mwaka 1

Mwaka 1 = siku 365 au 366
Mwaka 1 = wiki 52
Siku ina sehemu 2. Mchana na Usiku.

**Maswali:**

1. Mtoto wa Bwana na Bibi Mgeni hukaa shuleni kwa muda wa saa 4 na nusu.
   Je hizo ni dakika ngapi?
2. Toka Kijiji cha Upeo hadi Kijiji cha jirani Mwenyekiti alitumia

muda wa masaa 2 kwenda tu. Je kwenda na kurudi alitumia muda gani?

3. Mwaka mmoja una wiki 52. Je miaka 6 kuna wiki ngapi?

4. Kijiji chetu kiliuza nazi 3456 katika hizo ilionekana kuwa nazi 950 ni mbovu. Je nazi nzima zilikuwa ngapi?

## SOMO LA 26

**Kusudi la Somo:**

- Magonjwa ya minazi
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, hesabu na kujibu maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi na maneno ya somo.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu magonjwa ya minazi

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma sentensi na maneno ya somo kwa kutumia ubao kadi na ubao wa chaki.
- Fuata hatua za kujibu maswali ya somo la kwanza

: Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo la 26
- Fuata hatua za kujibu maswali ya somo la kwanza

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Wazo la eneo siyo geni kwa wanakisomo. Kitu muhimu ambacho wanapaswa **kufahamu** ni jinsi ya kutafuta eneo la kitu. Wanafahamu kuwa hatua 70 kwa 70 ni karibu eka 1. Hivyo wazo la eka wanafahamu. Eka 2½ ni sawa na hekta moja.

| | | Hatua 20 | Hatua 35 |
|---|---|---|---|
| 70 | Eka 1 | Eka 1 | ½ eka |
| | Hatua 70 | Hatua 70 | mita **35** |

Somo hili linafaa lifanywe kwa vitendo, ili **wazo la hekta lifahamike.**

**Wafahamu:**

1. Eka moja ni hatua 70 kwa 70. Eneo hili unaweza kupanda miche 121.

2. Hekta 1 ni eka 2½. Eneo hili unaweza kupanda karibu miche 300.

Kutafuta eneo la kitu ambacho ni mraba au mstatili tunazidisha urefu mara upana.

**Toa mfano huu:** Urefu wa bustani ni meta 15 na upana ni meta 8. Je eneo la bustani ni nini?

Eneo lake ni meta za eneo 15 x 8

$m^2$ 120

Wazoeze kusema "mita za eneo".

**Maswali:**

1. Kitalu kina urefu wa mita 13 na upana mita 7. Je eneo lake ni nini?

2. Kijiji kimepanda migomba katika eneo la eka 5. Je ni sawa na eka ngapi?

3. Shule ya Msingi ya Upeo imepanda minazi katika hekta moja. Idadi ya minazi 143. Je kama wakiwa na hekta 4 watakuwa na minazi mingapi?

## SOMO LA 27

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 25 na 26
- Kufundisha kusoma sentensi na hesabu.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi za somo la 27

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

Majadiliano kuhusu somo la 25 na 26

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi za somo la 27.
- Fuata hatua za kusma za somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 27
- Fuata hatua za majadiliano za somo la 6

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

**Matumizi ya fedha:**

Mwalimu awafundishe wanakisomo kuhusu matumizi ya fedha

wapatazo. Waelezwe umuhimu wa kuandika kila fedha iingiayo na kila fedha itokayo. Waelezwe kuhusu umuhimu wa kuweka makadirio na matumizi. Waelezwe umuhimu wa kuweka fedha benki.

Mfano: Bwana na Bibi Mgeni waliipata Shs.950 kutokana na kuuza nazi zao.

Walikaa kitako walianza kupanga hivi:

| | |
|---|---|
| – Mchango wa Shule kwa watoto wao 3 kila mtoto Shs.20 | Sh. 60.00 |
| – Mchango wa jengo la Ofisi ya Chama | Sh.100.00 |
| – Ununuzi wa chumvi kilo 10 kila kilo Sh.3 | Sh. 30.00 |
| – Ununuzi wa sukari kilo 5 kila kilo Sh.11 | Sh. 55.00 |
| – Ununuzi wa saruji mifuko 2 kila mfuko Sh.100 | Sh.200.00 |
| – Walipeleka benki Shs.300 | Sh.300.00 |
| Jumla .......... | Sh.745.00 |

Fedha zilizobakia ni Shs. 950 − 745 = 205

Fedha hizi zilizobaki ziliandikwa katika daftari ya matumizi, na kila Bwana na Bibi Mgeni walipoamua kununua vitu waliandika katika daftari hiyo; aliandika hivi:–

| Tarehe | Mapato (Fedha zilibakia mikononi) | | Matumizi | |
|---|---|---|---|---|
| 1/3/85 | Urari wa kuanzia | Sh.205.00 | Mbegu za mtama .............. | Shs.15.00 |
| 15/3/85 | ........ .......... | | Unga wa ngano kilo 5 kila kilo Shs.12 ................ | Shs.60.00 |
| 21/3/85 | Kuuza madafu kila moja Shs.3.00 .......Shs. | | 60.00 | |
| 25/3/85 | Kuuza nazi 30 kila nazi Shs.5 | Shs.150.00 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | JUMLA | 415.00 | |
| | | 83.00 | Shs.83.00 |
| 1/6/85 | Urari wa kuanzia | Shs.332.00 | |

Waeleze wanakisomo umuhimu wa kutotumia fedha zaidi kuliko walizonazo.
Kutumia fedha zaidi kunasababisha kukopa na kujiingiza katika madeni.

**Maswali:**

1. Bibi Mgeni alikwenda sokoni na Shs.60 alinunua maharage kilo 2 kila kilo Shs.6.00
2. Machungwa 10 kila chungwa Shs.1.00 Shs. ..............................
3. Samaki 4 kila samaki Shs.4... Shs. ..............................
4. Ndizi 20 kila ndizi Shs.1 .... Shs ..............................
5. Binzari vibunda 1 kila kimoja Shs.1 .....Shs..............................
6. Vitunguu mafungu 2 kila fungu Shs.3/= ..............................

Je jumla alilipa Shs. Ngapi?

Je Shs. ngapi zilibaki?

Bei ya ng'ombe 1 ni Shs.900, bei ya mbuzi 1 ni Shs.300 na bei ya kuku ni Shs.60. Nitarudishiwa Shs. ngapi kama nikinunua wanyama hawa na nina Shs.1,260 mfukoni?

## SOMO LA 28

**Kusudi la Somo**

- Ufugaji
- kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi - Ve, hesabu na maswali

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- Kadi za sentensi, maneno na silabi za somo
- picha nambari 13.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu ufugaji

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi maneno na silabi za somo
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- Kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Matumizi ya nukta katika hesabu

Mwalimu awaeleze wanakisomo matumizi ya alama hizi:

- ? alama ya kuuliza: **mfano** Je wazee mnafuata masharti ya afya bora?
- ! alama ya mshangao: **Mfano** Loo! minazi yangu imeliwa na mchwa:
- . alama ya nukta. Alama ya mwisho wa fungu la maneno.

Katika hesabu tunatumia nukta.

(i) Tunaweza kuandika Shs.12/50 kama 12.50

(ii) Tunaweza kuandika tarehe 3/4/85 kama 3.4.85 au 3-4-85

Waeleze wanakisomo kuwa:

1. Tukiambiwa senti 150 ni Shs. na senti ngapi
   Tunaandika Shs.1.50 hapa tunatenga shs. na senti

2. Tukiambiwa senti 2860 ni shs. na senti ngapi
   tunaandika shs.28.60

Wanakisomo wasomewe tarehe hizi halafu waandike kwa kutumia nukta.

1. Januari tarehe 10 mwaka 1985
Machi tarehe 7 mwaka 1986
Julai 7 mwaka 1954

## SOMO LA 29

**Kusudi la Somo:**

- Uvunaji na njia za kuhifadhi nazi
- Kufundisha kusoma sentensi, maneno, silabi - MSA hesabu na maswali.

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Ubao wa chaki
- kadi za sentensi, maneno na silabi za somo.
- Picha nambari 14.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano kuhusu uvunaji na njia za kuhifadhi nazi.

**Hatua ya Pili:**

Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi, maneno na silabi za somo.

- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Maswali:**

- kujibu maswali ya somo
- Fuata hatua za kujibu maswali za somo la kwanza.

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Wanakisomo wafundishwe namba toka 1,000 hadi 100,000

(i) Wanafahamu na kutambua namba toka 1 - 100
(ii) Wanafahamu na kutambua maelfu, mamia na mamoja
(iii) Wanafahamu kujumlisha, kutoa, kuzidisha na kugawanya maelfu, mamia makumi na mamoja.

**Wakumbushe:**

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Mamoja: | 1 - 9 |
| (ii) | Makumi: | 10 - 99 |
| (iii) | Mamia: | 100 - 999 |
| (iv) | Elfu: | 1000 - 9999 |

**Wakumbushe:**

(i) 11 = 10 + 1; 12 = 10 + 2; 13 = 10 + 3; 68 = 60 + 8 nk

(ii) 111 = 100 + 10 + 1; 112 = 100 + 10 + 2;
113 = 100 + 10 + 3; 168 = 100 + 60 + 8

(iii) 1111 = 1000 + 100 + 10 + 1;
2998 = 2000 + 900 + 90 + 8;
5864 = 5000 + 800 + 60 + 4;
88892 = 88,000 + 800 + 90 + 2

1 moja
10 kumi
100 mia
1,000 Elfu
10,000 kumi elfu
20,000 ishirini elfu
30,000 thelathini elfu
90,000 tisini elfu

**Fundisha:**

$$\begin{array}{r} 90{,}000 \\ +\,10{,}000 \\ \hline 100{,}000 \\ \hline \end{array}$$

Namba hii 100,000 tunaita **mia moja elfu** au kwa jina lingine **LAKI MOJA**, na 50,000 ni nusu laki.

**Vitendo:** Wanakisomo waandike kwa tarakimu namba hizi.

1 Sabini elfu (70,000)
1. Themanini elfu (80,000)
3. Laki mbili (200,000)
4. Laki nne (400,000)

## SOMO LA 30

**Kusudi la Somo:**

- Marudio ya somo la 28 na 29
- Kufundisha kusoma sentensi na hesabu

**Vifaa na Vielelezo:**

- Ubao wa kubandika kadi
- Kadi za sentensi za somo la 30 - marudio.
- Picha nambari 13 na 14.

**Jinsi ya Kufundisha Somo:**

**Hatua ya Kwanza:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 28 na 29.

**Hatua ya Pili:**

**Kusoma:**

- Kusoma kwa kutumia ubao wa kadi na ubao wa chaki, sentensi za somo la marudio.
- Fuata hatua za kusoma za somo la kwanza.

**Hatua ya Tatu:**

**Majadiliano:**

- Majadiliano ya somo la 30 la marudio.
- Fuata hatua za majadiliano za somo la 6

**Hatua ya Nne:**

**Hesabu:**

Rudia hesabu za somo la ishirini na tisa.

**Marudio:**

Tumekwisha fika mwisho wa kitabu, hivyo inatubidi turudie mada zote za hesabu zilizoko katika kitabu cha pili.

**Mada hizi:** (i) Kutambua mamoja 1 - 9
(ii) Kutambua makumi 10 - 99
(iii) Kutambua mamia 10 - 999

Kujumlisha mamoja tu: k.m. 3 + 4 = 7
Kujumlisha makumi na mamoja k.m.

$$\begin{array}{r} 13 \\ +14 \\ \hline \end{array}$$

Kujumlisha mamia, makumi na mamoja
k.m.

$$\begin{array}{r} 113 \\ +114 \\ \hline \end{array}$$

**Kujumlisha** maelfu, mamia, makumi, mamoja k.m.

$$\begin{array}{r} 1364 \\ +2133 \\ \hline \end{array}$$

**kutoa, kuzidisha** na **kugawa maelfu** n.k.

$$\begin{array}{r} 14 \\ \times 2 \\ \hline \end{array} \qquad \begin{array}{r} 114 \\ 2 \\ \hline \end{array} \qquad \begin{array}{r} 151 \\ +347 \\ \hline \end{array} \qquad \begin{array}{r} 256 \\ -144 \\ \hline \end{array}$$

$$2\overline{)684}$$

Rudia hesabu za vipimo: Uzito gramu, kilo na tani

gramu 1000 = kilo 1
kilo 1,000 = tani 1

Toa hesabu za kujumlisha, kutoa, kuzidisha na kugawanya zihusuzo vipimo: k.m.kilo

$$\begin{array}{r} 14 \\ +15 \\ \hline \end{array} \qquad \begin{array}{r} \text{kilo } 15 \\ \times\ 3 \\ \hline \end{array}$$

**Vipimo vya urefu:** Sentimita, mita, kilomita
sentimita 1,000 = mita 1
Sentimita, mita, kilomita
sentimita 1,000 = mita 1.
mita 1,000 = kilomita 1

Toa mifano wa kujumlisha, kutoa, kuzidisha, na kugawa kuhusu vipimo vya urefu.

**Ujazo:** Dakika, saa, siku, wiki, mwezi, mwaka,

dk. 60 = saa 1
saa 24 = siku 1
Siku 7 = wiki 1
wiki 4 = mwezi 1
miezi 12 = mwaka 1

Mwaka 1 = siku 365 au 366.

Wanakisomo wajifunze majina ya miezi na jinsi ya kuandika tarehe k.m. Januari 12 1985. tunaandika 1.1.1985 au 1/1/85. wanakisomo wajue miezi yenye siku 30 na ile yenye siku 31.

**Uwekaji wa fedha:** Rudia jinsi ya kuandika mapato na matumizi na kutafuta urari wa kuanzia.

**Rudia** - laki moja

ELIMU HAINA MWISHO